

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA



TAARIFA KWA UMMA

1. Tunapenda kutaarifu umma kuwa Mahakama imekamilisha mfumo wa kieletroniki wa kutunza taarifa za mawakili kuhusu usajili wao na sifa zao. Mfumo huo kwa sasa uko tayari kwa matumizi ya umma ambapo unaweza kuthibitisha iwapo wakili wako anafanya kazi kihalali. Mfumo huu unalenga kudhibiti mawakili vishoka na wale wanaofanya kazi bila kuwa na leseni.
2. Tunapenda kuufahamisha umma pia kwamba ni kosa kwa wakili kufanya kazi bila kuwa na leseni ya uwakili na iwapo atafanya hivyo uwakilishi wake Mahakamani au kazi yoyote aliyoifanya ni batili.
3. Ili kuthibitisha kama wakili anafanya kazi kihalali, tembelea mfumo na ufanye yafuatayo:-
 - i. Kuingia katika **"browser"** kwenye simu au kompyuta yako na uandike tams.judiciary.go.tz
 - ii. Browser itafunguka na kuonyesha **"Mjue wakili"**
 - iii. Andika katika kisanduku chini ya maneno hayo jina la wakili unayetaka kufahamu habari zake. Unaweza pia kutumia namba yake ya usajili (Roll number) kama unaifahamu
 - iv. Kama wakili ana leseni hai ya uwakili itatokea picha yake katika rangi ya bluu ikiambatana na maneno **"anaruhusiwa"**. Kama hana leseni hai itaandika **"haruhusiwi"** na picha yake itakuwa katika rangi nyekundu.
 - v. Kama mfumo umeonyesha wakili haruhusiwi, tafadhali usifanye naye biashara yoyote.
4. Mfumo umejengwa kwa lugha ya Kiswahili lakini unaweza kubadilika kuwa kwa Kiingereza. Tafadhali bonyeza maneno "EN" upande wa juu kulia kwako.
5. Mfumo unafikika pia kupitia tovuti ya Mahakama ambayo ni www.judiciary.go.tz (angalia upande wa kulia wa tovuti).


E. G. Mrangu

Kny: MSAJILI
MAHAKAMA KUU

MSAJILI
MAHAKAMA KUU
DAR-ES-SALAAH

Nakala:

1. Jaji Mkuu
2. Jaji Kiongozi
3. Msajili Mkuu
4. Mtendaji Mkuu